# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

*(Imetolewa chini ya Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari,2023)*

**12 MEI, 2025**

# YALIYOMO

*Ukurasa*

**YALIYOMO** .......... i
**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... ii
**ORODHA YA CHATI** .......... iii
**SEHEMU YA KWANZA** .......... 1
1.0 **UTANGULIZI** .......... 1
1.1 Maelezo ya Jumla .......... 1
1.2 Muundo wa Taarifa .......... 1
1.3 Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi .......... 2
1.3.1 Msingi wa Taarifa .......... 2
1.3.2 Mbinu Zilizotumika .......... 2
1.3.3 Wigo na mipaka ya Taarifa .......... 3
1.4 Majumuisho ya Sehemu .......... 3
**SEHEMU YA PILI** .......... 5
2.0 **MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI** .......... 5
2.1 Maelezo ya Jumla .......... 5
2.2 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 .......... 5
2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati .......... 6
2.2.2 Utekelezaji wa Kazi Zilizopangwa .......... 8
2.2.3 Ukusanyaji wa Mapato .......... 10
2.2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo .......... 13
2.2.5 Mwenendo wa upatikanaji wa fedha .......... 15
2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 .......... 17
2.3.1 Makadirio ya Mapato .......... 18
2.3.2 Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo .......... 21
2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida .......... 22
3.0 **MAONI NA USHAURI WA KAMATI** .......... 24
3.1 Maelezo ya Jumla .......... 24
3.2 Maoni ya Kamati .......... 24
3.3 Ushauri wa Kamati .......... 25
3.4 Hitimisho .......... 27
**KIAMBATISHO NA 1:** .......... 30
**KIAMBATISHO NA 2:** .......... 37

**ORODHA YA MAJEDWALI**

**Jedwali Na. 1:** Makadirio na Ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka 2024/2025 ....10

**Jedwali Na. 2:** Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli kwa Kipindi cha Kuanzia mwaka 2021/2022- 2024/2025....12

**Jedwali Na. 3:** Mchanganuo wa Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 kwa Wizara ya Elime, Sayansi na Teknoloja 15

**Jedwali Na. 4:** Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Elime, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2024/2025 na Mwaka 2025/2026 ....19

**Jedwali Na. 5:** Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2024/2025 na Mwaka 2025/2026....22

## ORODHA YA CHATI

**Chati Na. 1:** Taswira ya Uwiano wa Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 ....................................................11

**Chati Na. 2:** Mwenendo wa Ufikiaji wa Lengo la Makusanyo ya Maduhuli kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 -2024/2025..........................12

**Chati Na. 3:** Mchanganuo wa Upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2024/2025 kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ...............17

**Chati Na. 4:** Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2024/2025 na 2025/2026......20

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2025/2026. Hatua inazingatia masharti ya Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufatilia mtiririko wa Taarifa hii, naomba kubainisha muundo wake ambao umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge. Kwa kufanya hivyo, vigezo vilivyozingatiwa katika uandishi wa Taaarifa hii vimebainishwa na uonesha uhalali wa uchambuzi, maoni na ushauri unaotolewa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa maelezo hayo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kama ifuatavyo: -

(i) **Sehemu ya Kwanza** inaeleza msingi, mbinu na wigo wa kazi ya Kamati katika uchambuzi wake;

(ii) **Sehemu ya Pili** inaeleza matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi;

(iii) **Sehemu ya Tatu** inahusu maoni, ushauri na hitimisho.

## 1.3 Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi

### 1.3.1 Msingi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa Taarifa hii ni Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la Februaari, 2023. Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge imeweka ufafanuzi wa majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge ikiwemo kamati hii. Kifungu cha 6(7) (a) cha Nyongeza ya nane ya Kanuni za Bunge, kinaipa Kamati hii jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka makadirio haya yajadiliwe na Kamati kabla ya kuwasilishwa Bungeni leo. Naomba kulihakikishia Bunge hili kuwa masharti hayo yalitimizwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuzingatia masharti ya Kanuni za Bunge, mapema asubuhi ya leo, taarifa hii iliwekwa mezani kwa mujibu wa Kanuni ya 118(5) ya Kanuni za Bunge. Na sasa, umenipa nafasi hii adhimu ili niweze kuwasilisha Taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge.

### 1.3.2 Mbinu Zilizotumika

**Mheshimwa Spika**, ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii inabinisha mbinu zilizotumika. Madhumuni ya kuonesha mbinu ni kuipa taarifa hii msingi wa kuwa rejea madhubuti ambayo inakidhi vigezo vya uadilifu uliozingatiwa na kupata maoni na ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi, Kamati ilitumia mbinu zilizojumuisha kupokea maelezo ya Waziri, kuhoji

mambo yaliyojitokeza na kupokea majibu ya mtoa hoja. Njia kuu iliyotumika ni ulinganisho wa maudhui na hali halisi. Kwa kufanya hivyo, imekuwa yenye msingi na ushauri unaozingatia hali halisi kiutekelezaji.

### 1.3.3 Wigo na mipaka ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, wigo na mipaka ya maudhui ya taarifa hii umetokana na kazi za Kamati zilizoainishwa katika Kanuni za Bunge. Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 unajikita kwenye malengo yaliyokuwa yamepangwa, ukusanyaji wa mapato na upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa kwa upande wa Mwaka 2025/2026, uchambuzi unagusa vipaumbele vya Wizara, makadirio ya mapato na matumizi.

**Mheshimiwa Spika**, mambo yote nje ya maeneo niliyoyataja hayatakuwa sehemu ya Taarifa hii. Lengo ni kuzingatia masharti ya Kanuni ya 71(1) ya Kanuni za Bunge kuhusu mambo yasiyoruhususiwa kuzungumzwa wakati wa hoja hii. Kwa ujumla wigo na mipaka hiyo ni muhimu na unafanikisha azma ya Bunge kuendeshwa kwa taratibu bora na madhubuti.

## 1.4 Majumuisho ya Sehemu

**Mheshimiwa Spika**, Jumla ya yote katika sehemu ya kwanza, Taarifa imetoa ombi la kuwasilisha rasmi taarifa hii katika hatua za Bunge kushughulikia hoja ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Pamoja na hilo, sehemu hii imeonesha ilivyozingatia masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo

wa Taarifa za Kamati ikiwemo Kamati hii. Kanuni iliyozingatiwa ni Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, misingi iliyotajwa kwenye sehemu ya kwanza ni Kanuni ya 137 iliyoanzisha Kamati na kufafanua majukumu yake kwenye Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Vilevile Kanuni ya 118 inayohusu taratibu za kushughulikia makadirio ya mapato na matumizi na Kanuni ya 142 inayohusu muundo wa Taarifa zimerejewa kwa Kanuni hizo, makadirio haya yalifanyiwa uchambuzi, mapema asubuhi, Taarifa imewekwa mezani na sasa inasomwa rasmi.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 142 (b) inaonesha kuwa sehemu ya pili ya Taarifa hii inapaswa kutoa maelezo kamili kuhusu mambo yote yaliyochambuliwa na Kamati kwa kuzingatia masharti hayo, sehemu hii itakuwa na maaelezo kuhusu mambo makuu mawili. Mambo hayo ni: -

(i) Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(ii) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huo ulifanyika kwa ulinganisho kama ilivyoelekeza Kanuni ya 117 (1) na 117 (2) za Kanuni za Bunge. Hivyo, uchambuzi huo unajenga msingi wa maoni na ushauri wa Kamati.

### 2.2 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** lengo la uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti limeelezwa katika Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge kwa mujibu wa Kanuni hiyo, lengo ni kufanya ulinganisho na makadirio kwa Mwaka wa Fedha unaofuata. Tafsiri yake ni kuwa uzoefu wa utekelezaji utumike kujenga maoni kuhusu makadirio kwa Mwaka wa Fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni hayo, sehemu hii inachambua mambo matano ambayo ni: -

(i) Uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati;

(ii) Utekelezaji wa kazi zilizopangwa;

(iii) Ukusanyaji wa mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(iv) Utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na

(v) Upatikanaji wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huo utajenga vigezo vya kutumika kufanya tathmini ya uhalisia wa makadirio ya mapato na matumizi. Hatua hiyo ni ya muhimu kwa uamuzi bora wa Bunge.

### 2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kuonesha uwajibikaji Bungeni, sehemu hii inaripoti kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa kamati. Nilikumbushe Bunge lako tukufu kuwa, tarehe 07 Mei, 2024, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo makuu kumi (10) kuhusiana na Wizara hii. Ushauri huo ulitolewa katika Kikao cha Ishirini cha Mkutano wa kumi na Tano wa Bunge wakati Bunge lilipopitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.[1]

[1] Taz. Taarifa Rasmi ya Majadiliano ya Bunge tarehe 07 Mei, 2025,

**Mheshimiwa Spika,** lengo la kuripoti jambo hili ni kuliwezesha Bunge kujadili hoja iliyowasilishwa Bungeni likiwa na kumbukumbu muhimu kuhusu ushauri uliotolewa Mwaka wa Fedha unaokwisha. Kufanya hivyo kunaliwezesha Bunge kuwa na tathmini endelevu ya utekelezaji wa Wizara hii na mwenendo wa sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati inaonesha kuwa sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati umefanyiwa kazi. Kwa mfano, Kamati ilishauri kuwa, changamoto ya uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunza itatuliwe kwa kuongeza bajeti kwa ajili hiyo. Taarifa ya Waziri ilionesha kuwa ushauri huo ulizingatiwa kwa kuongeza kiasi cha **Sh. bilioni 91.9** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa. Aidha, **Sh. Bilioni 21.3** zinaongezwa kwenye bajeti kwa Mwaka 2025/2026 kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo 65 vya VETA. Taarifa zaidi ilionesha kuwa **Sh. Bilioni 7** zinatengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia ikiwemo mitambo na mashine.

**Mheshimiwa Spika**, ushauri mwingine umeanza kuzingatiwa na upo katika mchakato maalumu. Kwa mfano, Kamati ilishauri kuwa vigezo vya utoaji wa mikopo ya Elimu ya Juu vifanyiwe mapitio kwa lengo la kuwa na vigezo visivyosababisha malalamiko na vyenye tija katika azma ya Taifa. Majibu ya Serikali yameonesha kuwa ushauri huu umezingatiwa kwa kiasi kikubwa, kufikia hatua ya kusubiri maoni ya wadau. Taarifa ilionesha kuwa Serikali imekamilisha

mapitio ya muundo na utendaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Aidha, Serikali imeboresha vigezo vya utoaji wa mikopo ambavyo vitaanza kutumika kuanzia Mwaka wa Fedha 2025/2026 baada ya kuridhiwa na wadau.

**Mheshimiwa Spika**, hatua ya Serikali kusikiliza na kuzingatia ushauri unaotolewa Bungeni inastahili kupongezwa. Ni hatua ambayo inafanikisha lengo la Serikali kuwezesha ustawi wa watu kwa kuzingatia ushauri wa wananchi kupitia kwa wawakilishi wao.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ufafanuzi wa kina kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, **Kiambatisho Na. 02** kinaeleza zaidi. Lengo la ufafanuzi huo ni kubainisha namna Serikali ilivyozingatia na hatua iliyofikiwa.

### 2.2.2 Utekelezaji wa Kazi Zilizopangwa

**Mheshimiwa Spika**, wakati Bunge lilipopitisha na kuidhinisha bajeti ya Wizara hii, lilizingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa. Kwa sababu hiyo, Kamati ilitaka kujiridhisha na kiwango cha utekelezaji kilichofikiwa. Lengo ni kulijulisha Bunge matokeo ya utekelezaji wa bajeti katika kazi mbalimbali zilizopangwa kufanyika.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya utekelezaji wa kazi zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 yanapatikana katika Randama ya **Fungu 46 – Wizara** na **Fungu 18 – Tume ya Taifa ya UNESCO**. Uchambuzi wa taarifa hizo unaonesha mambo yafuatayao:-

(i) Baadhi ya kazi zilizopangwa kwa Mwaka 2024/2025 zinaendelea kufanyika hadi sasa kwa kuwa ni endelevu;

(ii) Baadhi ya kazi zimetekelezwa zikiwa zinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile uhaba wa Rasilimali muhimu;

(iii) Sehemu kubwa ya kazi zilizotekelezwa zinaendana na malengo yaliyokuwa yamewekwa.

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa kazi zinazoendelea ni kazi ya utekelezaji Sera na Mitaala, mapitio ya sheria zinazohusu utoaji wa elimu na mafunzo nchini pamoja na uandaaji wa miongozo inayohusika. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa, Sera ya Taifa ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 ilizinduliwa tarehe 01 Februari, 2025. Aidha, Mikutano mbalimbali na vyombo vya habari ni miongoni mwa njia zilizotumika kutoa elimu kwa umma kuhusu sera ya taifa ya Elimu na Mafunzo pamoja na mitaala ya ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa kazi zilizokabiliwa na changamoto ni utekelezaji wa mpango wa fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali (ufundi na ufundi stadi) katika shule za sekondari na vyuo vya amali. Taarifa ya Serikali ilionesha kuwa, kazi hiyo ilikabiliwa na uhaba wa walimu, wakufunzi na wahadhiri hususani katika masomo au fani za sayansi, hisabati na mafunzo ya amali.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto hizo, kazi zilizopangwa kwa Mwaka 2024/2025 zimetekelezwa. Ni maoni ya Kamati kuwa ili kuwa na mwendelezo mzuri wa kazi hizo, upo umuhimu wa kutatua changamoto zinazohusika.

### 2.2.3 Ukusanyaji wa Mapato


**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo kawaida ya bajeti kuwa na pande mbili. Mapato na matumizi, Bunge lilipitisha makadirio ya mapato ya Wizara hii. Kwa madhumuni ya uwajibikaji Kibunge, Kamati ilitaka kufahamu ukusanyaji wa mapato yaliyoidhinishwa. Muhtasari wa taarifa za ukusanyaji wa mapato unaonekana katika **Jedwali Na. 1** na picha ya hali halisi inatolewa kwenye **Chati Na. 1.**

**Jedwali Na. 1: Makadirio na Ukusanyaji wa Maduhuli kwa mwaka 2024/2025**

| CHANZO | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara/Vitengo | 9,700,537,000.00 | 6,301,274,501.06 | 64.96 |
| Taasisi | 667,598,605,074.83 | 371,121,898,270.84 | 55.59 |
| **Jumla** | **667,299,142,074.83** | **377,423,172,771.90** | **56** |

**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Chati Na. 1: Taswira ya Uwiano wa Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa fedha 2024/2025**




**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa mwenendo huo wa ukusanyaji wa mapato unaonesha yafuatayo: -

(i) Hadi kufikia Februari, 2025 kiasi kilichokusanywa ni Sh. **377,423,172,771.9** sawa na **asilimia 56;**

(ii) Mwenendo huu wa hali ya ukusanyaji wa mapato umekuwa kwa kiwango hicho au karibu na kiwango hicho kwa takriban miaka minne kuanzia 2021/2022 hadi 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, hali hiyo iliifanya Kamati kutathmini mwenendo huo kwa lengo la kubaini msingi wa hali hiyo.

**Jedwali Na. 2**, linadhihirisha mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa kipindi hicho kwa urahisi wa uchambuzi.


**Jedwali Na. 2 Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli kwa Kipindi cha Kuanzia mwaka 2021/2022- 2024/2025**

| MWAKA | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| 2021/2022 | 555,043,008,495.63 | 350,484,167,565.79 | 63 |
| 2022/2023 | 642,667,620,483.06 | 338,199,478,541.42 | 53 |
| 2023/2024 | 679,362,572,548.64 | 318,339,539,882.24 | 47 |
| 2024/2025 | 667,299,142,074.83 | 377,423,172,771.90 | 56 |

***Chanzo:*** *Taarifa za Kamati 2021/2022 – 2022/2023 na Randama ya Wizara 2024/2025*

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kuchambua mwenendo wa makusanyo, **chati Na. 2** inatoa taswira halisi.

**Chati Na. 2 Mwenendo wa Ufikiaji wa Lengo la Makusanyo ya Maduhuli kwa kipindi cha mwaka 2021/2022 -2024/2025**



**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha yafuatayo: -

(i) Mwaka 2021/2022 ambao ni wa mwanzo katika uchambuzi (base year) ukusanyaji ulikuwa wa kuridhisha kwa kuwa ulivuka nusu;

(ii) Miaka miwili iliyofuata, ukusayaji ulikuwa na mwenendo unaoshuka hadi kufikia **asilimia 47;**

(iii) Mwaka huu unaokwisha, mwenendo wa ukusanyaji umeanza kupanda ingawa bado si ishara ya kufikia lengo kwa kipindi kilichobaki.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huu unatoa misingi ya kuzingatia katika uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, kuna dalili kuwa lengo lililopangwa ama halikuwa halisi au ukusanyaji haukufanyika kwa ufanisi lakini kwa kuwa hali imekuwa hivyo kwa zaidi ya miaka miwili, kuna umuhimu wa kufanyia kazi lengo la makusanyo linalowekwa kwa Wizara hii.

### 2.2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya usimamizi wa Kibunge wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo, Kamati ilitaka kufahamu hatua za utekelezaji. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi mitatu miradi hiyo ni: -

(i) Mradi Na. 6350 – ukarabati na upanuzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam;

(ii) Mradi Na. 4382 – Ukarabati wa karakana za mafunzo, Hostel za wanafunzi, ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Teknolojia Dar es salaam (DIT); na

(iii) Mradi Na. 4315 – mradi wa kuendeleza Elimu ya Juu kwa ajili ya mabadiliko ya Kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** miradi hiyo inaendelea kutekelezwa ili kufikia malengo yaliyowekwa hata hivyo kuna changamoto mbili zilizobainika. Changamoto hizo ni kuchelewa kwa fedha za kugharamia miradi na kuwa nyuma ya Ratiba. Maelezo kamili ya hali ya miradi yanaelezwa katika **Kiambatisho Na. 01**.

**Mheshimiwa Spika,** hali ya jumla ya upatikanaji wa fedha za kugharimia miradi ya maendeleo inaonesha kuwa nzuri. Taarifa ya Waziri ilionesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2025, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 64 ya fedha zote za miradi. Uchambuzi zaidi ulionesha mambo yafuatayo:-

(i) Hali ya jumla ya upokeaji wa fedha za kugharamia miradi imekuwa nzuri kutokana na mchango wa fedha za nje kuliko fedha za ndani;

(ii) Upokeaji wa fedha za ndani hauoneshi mwenendo mzuri hadi kufikia mwezi Februari, 2025 fedha zilizopokelewa ni asilimia 55 tu.

(iii) Hali ya jumla ya utekelezaji wa miradi hiyo inaonekana kuwa nzuri pamoja na changamoto za upatikanaji wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa kuchelewa na usimamizi kutowezesha uzingatiaji wa ratiba ya miradi zinafaa kufanyiwa kazi. Aidha, uzoefu kuhusu changamoto hizo na masuala mengine kuhusu usimamizi wa miradi ni mambo ya kuzingatiwa katika bajeti ya mwaka 2025/2026.

### 2.2.5 Mwenendo wa upatikanaji wa fedha

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lilipopitisha bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 lilipitisha kiasi cha Sh. 637,287,706,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida (recurrent expenditure). Lengo la kiasi hicho lilikuwa ni kuwezesha ugharamiaji wa uendeshaji wa Wizara na mishahara ya watumishi. Taarifa iliyotolewa kwenye Kamati ilibainisha mwenendo wa upokeaji kama inavyoonekana kwa muhtasari kwenye **Jedwali Na. 3**.

**Jedwali Na. 3 Mchanganuo wa Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 kwa Wizara ya Elime, Sayansi na Teknoloja**

| AINA YA MATUMIZI | KIASI KILICHOIDHINISHWA | KIASI KILICHOPOKELEWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 85,225,031,000.00 | 368,412,483,674.74 | 63 |
| Mengineyo | 52,062,675,000.00 | 29,382,258,159.78 | 56 |
| **JUMLA** | **637,287,706,000.00** | **397,794,741,834.52** | 62 |

**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi taarifa hizo unaonesha mambo yafuatayo: -


(i) Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 kiasi kilichopokelewa kwa ujumla ni **asilimia 62** ikiwa ni karibu **asilimia 67** ya kipindi cha utekelezaji;

(ii) Kiasi kilichopokelewa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Wizara hadi kufikia mwezi Februari, 2025 ni **asilimia 56** tu.

(iii) Kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya mishahara hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 kilifikia asilimia kubwa zaidi ya asilimia za fedha ya matumizi mengineyo;

(iv) Uwiano wa bajeti ya mishahara na matumizi mengineyo wakati wa kupitisha bajeti kwa Mwaka 2024/2025, unatofautiana na uwiano wa namna hiyo katika Taarifa za utekelezaji kama inavyoonekana katika **Chati Na. 3**.

**Chati Na. 3 Mchanganuo wa Upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2024/2025 kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**




**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, tafsiri ya hali hiyo ni kuwa fedha za uendeshaji zimekuwa changamoto. Kwa kuwa hadi mwezi Februari, 2025 kiasi kilichopatikana ni asilimia 56 tu, ni wazi kuwa kwa kipindi cha Februari hadi Juni, 2025 uendeshaji utasuasua. Kamati ina maoni kuwa jambo hili linahitaji kufanyiwa kazi.

## 2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni 117 (2) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti kwa Kamati kulinganisha utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka unaoisha na makadirio kwa Mwaka wa Fedha unaofuata. Kwa kuzingatia masharti hayo, sehemu hii inafanya uchambuzi unaozingatia ulinganisho.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutumia mbinu ya ulinganisho kwa njia ya asilimia na uchambuzi wa mwenendo, mambo makuu yaliyowekewa mkazo ni: -

(i) Makadiirio ya mapato kwa mwaka 2025/2026;

(ii) Makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo; na

(iii) Makadirio ya matumizi ya kawaida (recurrent expenditure).

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huo unajenga msingi wa ushauri wa Kamati na ni taarifa muhimu kwa uamuzi wa Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa sababu hiyo, ufafanuzi unatolewa kama ifuatavyo: -

### 2.3.1 Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, hotuba ya Waziri iliyowekwa mezani mapema asubuhi ya leo kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (3) ya Kanuni za Bunge imetaja kiasi cha fedha kinachokadiriwa kuwa mapato. Kiasi hicho ni sawa na kiasi kilichoelezwa kwenye Kamati. Naomba kulijulisha Bunge matokeo ya uchambuzi wa kiasi hicho kwa njia ya ulinganisho kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 04 .**

**Jedwali Na. 4 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Elime, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2024/2025 na Mwaka 2025/2026**

| CHANZO | MAKADIRIO 2024/2025 | MAKADIRIO 2025/2026 | ONGEZEKO/PUNGUFU | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| **WIZARA** | 9,700,537,000.00 | 8,402,257,000.00 | 1,298,280,000.00 | **13.4** |
| **TAASISI** | 677,299,142,074.83 | 702,105,622,789.63 | 24,806.480,714.83 | **3.7** |
| **JUMLA** | **667,598,605,074.83** | **710,507,879,789.63.** | **42,909,274,714.8** | **6.4** |

**Chanzo:** Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** uchanbuzi uliofanyika unaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya mapato kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 yameongezeka kwa **asilimia 6.4** ikilinganishwa na Mwaka 2024/2025;


(ii) Makadirio ya mapato kati ya Wizara na Taasisi ake yameongezeka kwa asilimia tofauti. Wakati Wizara ina ongezeko la **asilimia 13.4**, taasisi zinaongezeko la **asilimia 3.7**;

(iii) Wakati ukusanyaji wa mapato kwa Mwaka 2024/2025 ulionesha ugumu wa kufikia lengo, makadirio ya mapato yameongezeka kwa **asilimia 6.4**

(iv) Wakati bajeti ya matumizi ya Wizara hii imeongezeka kwa **asilimia 24**, ongezeko la makadirio ya mapato haliendani na kiasi cha ongezeko la bajeti ya matumizi.

**Mheshimiwa Spika**, uchanganuzi huo unaonesha pia uwiano wa mchango wa mapato ya Wizara na taasisi zake kama inavyoonekana katika **Chati Na. 4**.

**Chati Na. 4 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2024/2025 na 2025/2026**




**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, kwa tafsiri ya uchambuzi huo, ni wazi kuwa uzoefu uliopatikana katika ukusanyaji wa mapato kwa Mwaka wa Fedha halikuzingatiwa. Kwa sababu hiyo Kamati ina maoni kuwa, ni vema upangaji wa bajeti uwe ukizingatia uzoefu unaopatikana kwa Mwaka wa fedha unaomalizika. Aidha, uhalisia wa vyanzo vya mapato usipozingatiwa, ukusanyaji wa mapato utatofautiana na lengo linalotokana na makadirio.

### 2.3.2 Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, makadirio ya bajeti ya maendeleo yanalenga kuwezesha gharama za utekelezaji wa miradi mbalimbali chini ya Wizara hii. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 kama ilivyo kuwa kwa mwaka 2024/2025 **Fungu 18 Tume ya Taifa ya UNESCO** halitekelezi mradi ya Maendelo. Fedha zote za miradi ya Maendeleo chini ya Wizara hii linakadiriwa katika **Fungu 46 kwa ajili ya WIzara na Taasisi zilizo chini yake**. Uchambuzi umeonyesha mambo yafuatayo;-

**(i)** Bajeti inayoombwa imeongezeka kwa takribani **asilimia 32.**

(ii) Ongezeko la Bajeti hiyo limetokana na ongezeko kubwa la fedha za nje ambazo zimeongezeka kwa **asilimia 90.3.**

(iii) Fedha za ndani zimeongezeka kwa **asilimia 14.8**.

(iv) Utegemezi wa fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni **asilimia 32** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo utegemezi ulikua ni **asilimia 22.2.**

**Mheshimiwa Spika**, tafsri ya matokeo ya uchambuzi huo inaonesha kuwa juhudi za Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan zimeongeza imani ya wabia wa maendeleo katika utekelezaji wa Miradi. Hata hivyo iwapo fedha hizo hazitopatikana, yamkini miradi hiyo itakwama.

### 2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, mapema asubuhi ya leo Mheshimiwa Waziri aliweka mezani hotuba yake inayoonyesha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaomba jumla ya shilingi **2,439,668,693,000** Kati ya fedha hizo **shilingi 691,854,522,000** ni makadirio ya matumizi ya kawaida kwa mafungu mawili, **Fungu -46 Wizara** na **Fungu 18 - Tume ya Taifa ya UNESCO**. Ili kuliwezesha Bunge kufanyia kazi makadirio hayo inavyostahili, Kamati imeweka muhtasari na mchanganuo wa fedha hizo katika **Jedwali Na 5**.

**Jedwali Na. 5 Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2024/2025 na Mwaka 2025/2026**

| AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2025/2026 | % ONGEZEKO/ PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 585,225,031,000 | 635,249,992,000 | 9 |
| Kawaida | 52,062,675,000 | 53,364,242,000 | 3 |
| Maendeleo | 1,328,042,674,000 | 1,747,814,171,000 | 32 |
| **JUMLA** | **1,965,330,380,000** | **2,436,428,405,000** | **24** |

***Chanzo:*** Usanifu wa Kamati kutokana na Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha mambo yafuatayo;-

(i) Makadirio hayo yameongezeka kwa **asilimia 8.1** ikilinganishwa na bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

(ii) Ongezeko hilo linaonesha kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026 unatarajiwa kuboreshwa kwa kuzingatia uzoefu wa mwenendo huo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**(iii)** Bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Tume ya Tafa ya UNESCO (Fungu 18) imeongezeka kwa **asilimia 12.4**

**Mheshimiwa Spika,** tafsiri ya matokeo ya uchambuzi huo inaonesha kuwa majukumu ya Tume ya Taifa ya UNESCO yamepewa kipaumbele zaidi ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha majukumu ya Wizara na Taasisi zake yamezingatiwa kwa kipaumbele zaidi ya ilivyokuwa mwaka wa fedha 2024/2025.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii, kwa mujibu wa Kanuni ya 142(c) ya Kanuni za Bunge, inafanya hitimisho baada ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati. Kwa ujumla, sehemu hii inachukua matokeo ya uchabuzi kwenye sehemu ya pili iliyozingatia msingi wa Taarifa kama ulivyofafanuliwa kwenye Sehemu ya kwanza.

### 3.2 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, maoni ya Kamati yanatokana na uchambuzi ulioripotiwa katika sehemu ya pili ya Taarifa hii. Moni hayo ni kama fuatavyo:-

(i) Kutokupatikana kwa fedha zlizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025, kunaathiri malengo na madhumuni ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka huo.

(ii) Mtiririko wa fedha kutoka HAZINA kwa ajili ya ukamilishaji wa vyuo 64 vya Elimu na Mafunzo Stadi (VETA) unachangia kutokamilika kwa wakati kwa ujenzi huo.

(iii) Upungufu wa walimu wa fani za Mkondo wa Amali na somo la elimu ya Biashara. Unachangiwa na kukosekana kwa mikakati maalum ya kuwapata walimu wa Amali na fani ya Biashara.

(iv) Upungufu wa fedha katika vyuo vya ualimu unaathiri mafunzo ya ualimu yanayoendana na mtaala mpya.

(v) Ongezeko la wanafunzi linalosababisha uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi ufikie 1:3 hadi 1:5 unaweza kurekebishwa na kuwa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja iwapo fedha za uchapaji zitapatikana kulingana na mahitaji.

(vi) Ukosefu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia vya kisasa, unaweza kuathiri lengo kuu la elimu nje ya mfumo rasmi unaotekelezwa kupitia Taasisi ya Elimu ya watu wazima kwa kushirikina na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

(vii) Motisha na maslahi bora kwa Makamu wakuu wa vyuo vikuu vya umma ni jambo muhimu kutokana na majukumu wanayotekeleza.

(viii) Utaratibu uliopo wa *Capitation grants* wa **shilingi 1000** kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kupitia **fungu 56** TAMISEMI kwa shule za msingi na sekondari unadhohofisha utendaji na ufanisi wa Wadhibiti Ubora. Aidha, mgawanyo wa majukumu unatambua jukumu la wadhibiti ubora kuwa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

### 3.3 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingata maoni ya Kamati ambayo ni mtazamo wa jumla kuhusu mambo manane niliyoyataja hapo juu Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitolewe kwa ukamilifu kabla ya tarehe 30 Juni, 2025.

(ii) Wizara ya Fedha ijitahidi kadri inavyowezekana kuwezesha mtiririko mzuri wa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa Ujenzi wa Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ambavyo ni vyuo 64 vya wilaya na kimoja cha Mkoa.

(iii) Wizara ya ELimu Sayansi na Teknolojia iandae mikakati maalum ya kuwapata walimu wa amali na fani ya Biashara.

(iv) Serikali iongeze fedha kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu ambavyo vitatoa na kuandaa mafunzo ya ualimu yatakayoendana na Mtaala mpya.

(v) Serikali iweke mikakati ya muda mfupi na mrefu ya kuandaa walimu wa masomo ya amali ili kuwawezesha wahitimu wa mafunzo ya amali kusoma kozi hizo na kuajiriwa kama walimu. Aidha mikakati ya kuwaendeleza walimu kupitia vyuo vikuu mbalimbali nchini iendelee kutekelezwa.

(vi) Serikali iendelee kutenga fedha za uchapaji wa vitabu kulingana na mahitaji ili kuimarisha uwiano wa kitabu na mwanafunzi hadi kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja (1:1). Aidha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itafute uwezekano wa kusambaza machapisho ya kieletroniki yaani (*e-books*)

kwa baadhi ya ngazi za elimu ili kupungiza uchapaji wa nakala Mango na pia kuhifadhi Mazingira.

(vii) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iandae mikakati ya kununua na kusambaza vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia masomo yote ikiwemo ujasiriamali, stadi za maisha na ufanisi mbalimbali. Lengo liwe kuwajengea uwezo wa kujifunza maarifa mapya kwa namna bora.

(viii) Serikali ichukue hatua madhubuti ya kushughulikia maslahi ya Makamu Wakuu wa Vyuo vya Umma nchini na kuhakikisha kuwa wanapata stahiki zao kulingana na vyeo vyao.

(ix) Serikali ihamishe ***capitation grants*** ya **shilingi 1000** kwa kila mwanafunzi wa shule ya msingi na sekondari kwa mwaka, kutoka **Fungu 56 - TAMSEMI** ambalo halihusiki na udhibti ubora na kupeleka Fungu 46 - Wizara ya ELmu, Sayansi na Teknolojia, ambalo linahusika na udhibiti ubora.

### 3.4 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, Nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Musa Ramadhani Sima, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Anastazia James Wambura, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Dr. Thea Ntara, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Ester Edwin Maleko, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Hassan Zidadu Kungu, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Kassim Ali Khamis, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Mohamed Said Issa, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Mwanakhamisi Kassian Said, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Nusrat Shaaban Hanje, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Rose Syprian Tweve, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Tunza Issa Malapo, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Yahya Ally Hamis, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wasaidizi wake, Mhe. Omary Shaban Kipanga (Mb), Naibu Waziri; na Prof. Carolyne Nombo, Katibu Mkuu wa Wizara hii, Dkt. Wilson Mahera, Naibu Katibu Mkuu – Elimu, Prof. Daniel Mushi - Naibu Katibu Mkuu - Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano

mkubwa walioipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongonzwa na Katibu wa Bunge *Ndg. Baraka Idephonce. Leonard,* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema katika wakati wote ilipokutana na hata wakati wa utayarishaji wa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili liijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Husna Juma Sekiboko, Mb

**MWENYEKITI WAKAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**

**YA ELIMU,UTAMADUNI NA MICHEZO**

12 Mei, 2025

## KIAMBATISHO NA 1:

## YATOKANAYO NA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOKAGULIWA

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa ziara za ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi husika. Uchambuzi wa taarifa hizo ulilinganishwa na hali halisi ya hatua zilizofikiwa pamoja na madhumuni ya kutekelezwa kwa miradi inayohusika. Naomba kutoa taarifa kuhusu matokeo ya ukaguzi na uchambuzi wake kama ifuatavyo:-

**a) Mradi Na. 6350. Ukarabati na Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Rehabilitation and Expansion project-UDSM)**

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa mradi huu unahusisha upanuzi na ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam katika Kampasi ya **Mwl. J.K. Nyerere.** Utekelezaji wake ni sehemu ya Mpango wa kukabiliana na upungufu mkubwa wa mabweni ya wanafunzi uliopo katika Chuo kikuu cha Dar es salaam. ambapo kwa sasa Chuo kina uwezo wa kulaza wanafunzi **11,115** ukilinganisha na wanafunzi **22,000** wanaohitaji malazi hii ni sawa na upungufu wa **asilimia 49.5.** Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza idadi ya wanafunzi watakao nufaika na huduma za Hosteli kuongezeka kutoka wanafunzi 3840 hadi kufikia wanafunzi 4416 hali itakayosaidia kupunguza idadi ya wanafunzi wanaoishi nje ya chuo.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ulikamilika Juni, 2022 na awamu ya pili ikitaraji kukamilika Mei, 2026. Kamati ilielezwa kuwa mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa awamu mbili awamu ya kwanza zilitengwa **shilingi 4,122,532,040.23** ikihusisha ujenzi wa mihimili ya jengo *(frame structure)* pamoja na kuezeka na ulikamilika 13 Juni, 2022. Awamu ya pili ikihusisha umaliziaji wa jengo na mazingira ya nje ya jengo *(Finishing and decoration)* ulitengewa kiasi cha **shilingi 9,462,459,651.45** na ulianza kutekelezwa 13 Mei, 2024 na unataraji kukamilika 12 Mei, 2026. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 mradi ulitengewa **shilingi 1,600,000,000** na ilielezwa kuwa hadi kufika Februari, 2025 mradi ulipokea Shilingi **680,490,038** sawa na **asilimia 43** huku utekelezaji wa mradi ukiwa **asilimia 5**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini changamoto kadhaa katika utekelezaji wa mradi huu ikiwa ni pamoja na ucheleweshwaji wa fedha kwa wakandarasi hali inayopelekea ucheweshwaji katika utekelezaji wa mradi. Kamati inaona ipo tija ya mradi huu kwa kuwa utasaidia kuongeza fursa ya upatikanaji wa huduma mbalimbali ikiwemo malazi ya hosteli na kupunguza adha wanazo kutana nazo wanafunzi wanaoishi nje ya Hosteli za Chuo. Ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali ihakikishe fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu zitolewe kabla ya mwaka huu wa fedha

2024/2025 kumalizika. Aidha, Kamati inaona upo umuhimu wa wakandarasi wazawa kutumika katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuhusisha wanafunzi ili waweze kupata ujuzi wa vitendo na kuongeza maarifa zaidi.

**b) Mradi Na 4382 Ukarabati wa karakana za mafunzo, Hosteli za wanafunzi, Ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia. Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni sehemu ya mradi wa kujenga Ujuzi kwa maendeleo na kuimarisha ushirikiano wa Kikanda katika Afrika Mashariki **(EASTRIP)** ukiwa na lengo la kimkakati la kuboresha Elimu ya Ufundi na Mafunzo katika ukanda wa Afrika Mashariki ukihusisha nchi tatu za Tanzania, Ethiopia na Kenya. Mradi unafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa **asilimia 100** kupitia mkopo wa Benki ya Dunia. Mradi huu kwa ujumla umekadiriwa kugharimu **Shilingi 74,035,000,000** hadi kukamilika kwake ikihusisha uanzishaji wa Vituo viwili vya umahiri katika Taasisi ya Teknolojia Da r es salaam. Aidha, kila kituo kimetengewa kiasi cha **Shilingi 37,017,500,000** ikiwa ni kituo cha Umahiri wa TEHAMA Kampasi ya Dar es salaam na Kituo cha Umahiri wa uchakataji Ngozi na Teknolojia zinazoshabihiana kampasi ya Mwanza.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali ilitenga kwa mradi wa EASTRIP RAFIC **Shilingi 20,222,375,502** na hadi kufikia Februari, 2025 zilikuwa zimepokelewa **Shilingi 9,139,841,088** na mradi wa EASTRIP CELPAT zilitengwa **Shilingi**

**25,486,873,836.00** na hadi kufikia Februari, 2025 zilikuwa zimepokelewa **shilingi 33,212,150,465.00** sawa na **asilimia 89.7.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa ujenzi wa vituo hivi viwili utafanyika sambamba na kuongeza uwezo wa taasisi katika kutoa mafunzo ya elimu ya ufundi hapa nchini na ukanda wa Afrika Mashariki. Mradi utahusisha kuimarisha uwezo wa Taasisi katika usimamizi na menejimenti, kuhuisha mitaala, kuendeleza walimu na wafanyakazi waendeshaji, ununuzi wa vifaa bora na vya kisasa vya kufundishia na kujenga miundombinu ambapo ilielezwa kuwa takribani **asilimia 80** ya fedha zote za mradi zitatumika hii ikihusisha ujenzi wa majengo ya kufundishia, ofisi, mabweni na karakana za kufundishia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kwamba Kampasi ya Dar es Salaam ujenzi unajumuisha majengo mawili ambayo ni Jengo la RAFIC la ghorofa 5 lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,800 lenye maabara, vyumba vya mihadhara, madarasa, kumbi za mikutano, chumba cha ubunifu, chumba cha matengenezo ya tarakirishi *(computer)* na ofisi za wafanyakazi. Ujenzi unahusisha pia bweni la ghorofa mbili lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 325.

**Mheshimiwa Spika,** Kampasi ya Mwanza ujenzi umegawanyika katika awamu mbili ikihusisha ujenzi wa jengo la Taaluma, jengo la kufundishia na mabweni mawili huku awamu ya pili ikihusisha ujenzi wa jengo la uchakataji

wa ngozi pamoja na mfumo wa usafishaji wa majitaka *(effluent treatment plant*). Hadi kufikia 18 Machi, 2025 mradi kwa awamu ya kwanza ulikua umefikia **asilimia 81** na awamu ya pili **asilimia 57** ujenzi kwa awamu zote mbili umegharimu **shilingi 26,843,347,993.15**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini utekelezaji wa Mradi huu unakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo, wakandarasi kuchelewa kukamilisha mradi kwa wakati, kwa kuwa lengo la mradi huu ni kuimarisha ufanisi wa mafunzo kwa wanafunzi pamoja na malazi hivyo kukamilika kwa wakati kwa mradi huu kutasaidia Chuo kuondokana na changamoto hizo hasa muhula mpya wa masomo utakapoanza. Aidha, hadi kufikia Februari 2025 kiasi cha **shilingi 385,879,303** kilikuwa kimepokelewa sawa na **asilimia 100** kwa ajili ya ukarabati wa karakana ya Mekanika na ununuzi wa vifaa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam inaendelea na mpango wa ukarabati wa karakana ya Idara ya Uhandisi wa mitambo *(Mechanical enginnering),* pamoja na ununuzi wa mitambo ya kisasa, ili kuimarisha ufanisi wa mafunzo yanayotolewa kwa wanafunzi. Hata hivyo Kamati haijaridhishwa na utekelezaji wa mradi huu kwani hadi kufikia Machi, 2025 mradi huu ulikuwa umefikia **asilimia 20** tu.  Ni rai ya Kamati kuwa Serikali isimamie ipasavyo utekelezaji wa mradi huu ili ukamilike kwa wakati.

c) **Mradi Namba 4315: Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Juu kwa ajili ya Mabadiliko ya kiuchumi (higher Education for economic Transformation Project – HEET)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa maabara, karakana na madarasa katika chuo Kikuu cha Ardhi. Kamati ilielezwa kwamba utekelezaji wa mradi huu utagharimu jumla ya Dola za kimarekani **29,000,000.** Aidha, Kiasi cha **Dola 22,582,190** sawa na **asilimia 77.9** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Kampasi ya Dar es Salaam na Mwanza.

**Mheshimiwa Spika,** Kampasi ya Dar es Salaam chuo kitajenga majengo manne ikiwemo madarasa, maabara, studio na karakana. Ujenzi wa majengo hayo umefikia **asilimia 80** na unataraji kukamilika Julai, 2025. Kampasi ya Mwanza ilielezwa wamekamilisha upatikanaji wa Mshauri Elekezi wa kusimamia majengo matano yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,140 na watumishi 131. Aidha, majengo hayo yatahusisha ujenzi wa vyumba vya madarasa nane, studio vyumba vinne, ofisi za watumishi, nyumba za watumishi na zahanati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini mradi uliongezewa muda wa ziada wa miezi mitano hadi ifikapo Julai, 2025 utakua umekamilika. Kamati inaushauri Serikali kuwa ni vyema mradi huu usimamiwe kikamilifu na ukamilike ndani ya muda ulioongezwa ili kuongeza idadi kubwa ya wanafunzi

watakao jiunga na masomo katika chuo hiki na hivyo kuongeza tija ya elimu nchini.

## KIAMBATISHO NA 2:

## UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilishauri masuala mbalimbali ambapo maelezo ya Wizara kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri huo ni kama ifuatavyo: -

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1. | Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Hata hivyo, Kamati inatoa maoni yafuatayo:<br><br>(i) Serikali iweke umakini katika usimamizi wa Miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha ili kuwezesha kupatikana kwa thamani halisi ya fedha na kukamilisha haraka na kwa wakati | (i) Serikali inatambua umuhimu wa usimamizi makini katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa lengo la kupata thamani ya fedha. Kwa kulitambua hili, Serikali imeendelea kuimarisha ufuatiliaji na tathmini kwa kuanzisha Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini ili kuhakikisha kuwa miradi yote ukiwemo mradi katika Chuo cha Nelson Mandela, inatekelezwa kwa thamani halisi ya fedha iliyokusudiwa. Aidha, Serikali imekuwa ikitumia Wataalamu Elekezi wa ndani ili |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | miradi hiyo ikiwemo Mradi unaotekelezwa katika chuo cha Nelson Mandela; | kuhakikisha miradi yote inatekelezwa kwa ubora zaidi kwa lengo la kuleta matokeo tarajiwa. Mradi wa chuo cha Nelson Mandela hadi Februari 2025 umepokea **Shilingi Bilioni 3** na mradi umefikia **asilimia 74** na katika mwaka wa fedha 2025/26 **Shilingi 2,500,000,000.00** zimetegwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa maktaba na jengo la utawala na ukarabati wa miundombinu. |
| | (ii) Kamati inasisitiza kuongeza kasi ya utolewaji wa fedha za miradi mbalimbali inayoendelea ya ujenzi na ukarabati wa Vyuo Vikuu na kuwepo na usimamizi mzuri wa miradi hiyo ili ikamilike kwa wakati na kuweza kutimiza lengo la kuanzishwa kwake; na | (ii) Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi wa miradi pamoja na kuongeza kasi ya utoaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyuo vikuu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/25 jumla ya **Shilingi 152,739,188,560.00** zilitengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | miundombinu ya vyuo vikuu (ikiwemo ujenzi wa kampasi mpya 16) ambapo hadi Februari 2025 vyuo vikuu vimepokea jumla ya **Shilingi 154,538,570,315.83** |
| | (iii) Ujenzi wa Vyuo vya VETA unaoendelea katika Mikoa mbalimbali nchini uzingatie upatikanaji wa maeneo makubwa ambayo yatakidhi ujenzi wa miundombinu ya kisasa na mahitaji ya baadaye. | 1 Serikali imepokea ushauri. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia mpango wa utengaji wa maeneo ya ujenzi wa vyuo vya VETA ambapo ni utengaji wa ekari 20 au zaidi kwa ngazi ya wilaya na ekari 50 au zaidi kwa ngazi ya mkoa. Ujenzi wa vyuo 65 vya VETA unaoendelea umezingatia vigezo hivyo. |
| 2. | Kamati imebaini kuwa, bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia sehemu kubwa ni bajeti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ambayo ni **asilimia 60.33** ya bajeti ya maendeleo. Hali hii | Serikali imepokea ushauri na itaendelea kuongeza bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha. Aidha, Serikali itaendelea kuandaa maandiko mbalimbali kwa ajili ya kuvutia vyanzo vipya vya mapato pamoja |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | inakwamisha dhamira ya kuimarisha miundombinu na taratibu za nchi kupata watanzania walioelimika na wanaoendelea kujielimisha na kuongeza tija katika maendeleo ya Taifa. **Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya Wizara ili kuboresha na kuimarisha Sekta ya Elimu na kukuza maendeleo ya Taifa.** | na kushirikiana na sekta binafsi na asasi zisizo za Serikali ili kuboresha na kuimarisha Sekta ya Elimu na kukuza maendeleo ya Taifa. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 wizara inakadiriwa kutumia bajeti ya **Shilingi 2,436,428,405,000.00** sawa na ongezeko la asilimia 24 ukilinganisha na bajeti 2024/25 ya **Shilingi 1,965,330,380,000.00** |
| 3. | Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza Sera ya kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi nchini. Ujenzi huu ukikamilika utaongeza fursa ya upatikanaji wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa lengo la kuwawezesha wananchi hususan vijana kupata ujuzi utakaowawezesha kujiajiri au kuajiriwa na hivyo kupunguza tatizo la ajira | (i) Serikali imeendelea kuongeza bajeti ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/24 **Shilingi bilioni 74.77** zilitengwa na kwa mwaka 2024/25 **Shilingi bilioni 105.9** zimetengwa ikiwa ni ongezeko la **Shilingi bilioni 31.17** kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za VETA ikiwemo vyuo 29 vya VETA vilivyokamilika na ujenzi wa VETA 65 awamu ya I unaoendelea. |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | nchini. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo kwa ufinyu wa Bajeti, idadi ndogo ya Wakufunzi, upungufu wa vitendea kazi na ukosefu wa zana za kufundishia na kujifunzia. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inasisitiza yafuatayo yafanyike ili kuboresha mpango wa ujenzi wa vyuo:<br>(i) VETA iongezewe bajeti kwa ajili ya uendeshaji wa vyuo vipya 29 vilivyoongezeka ili viweze kutoa mafunzo na kuleta tija iliyokusudiwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwezesha Watanzania hususan vijana kupata ujuzi | Kwa mwaka wa fedha 2025/26 **Shilingi bilioni 202.6** zimetengwa ikiwemo **Shilingi bilioni 89.4** kwa ajili ya uendeshaji na **Shilingi bilioni 91.9** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na **Shilingi bilioni 21.3** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa VETA 65.<br><br>Vilevile, Serikali imetenga kiasi cha **Shilingi bilioni 7** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia ikiwamo mitambo na mashine. Aidha, Serikali itaendelea kuongeza bajeti kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha ili kuimarisha utendaji wa VETA. |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | utakaowawezesha kutekeleza shughuli zao za kiuchumi na kujiajiri. Hata hivyo Wizara iweke mpango madhubuti kwa ajili ya uendeshaji wa vyuo vinavyoendelea kujengwa ambapo vikikamilika Taasisi hii itakuwa na jumla ya Vyuo **145** kutoka **51** vilivyokuwepo hapo awali | |
| | (ii) Ujenzi wa vyuo vya VETA uende sambamba na kuajiri wakufunzi wa mafunzo ya ufundi kulingana na mahitaji pamoja na vitendea kazi hususani karakana za ufundi. | (ii) Serikali inatambua umuhimu wa rasilimali watu katika utoaji wa Mafunzo ya ufundi stadi. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali imeajiri wakufunzi 35 na watumishi mwega 32 ambao wameshapangiwa vituo vya kazi. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2024/25 Serikali imeajiri watumishi **247 wakiwemo wakufunzi 143 na watumishi** |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | **mwega 104** kwa ajili ya usimamizi na utoaji wa mafunzo katika vyuo vya ufundi stadi kwa ajili ya vyuo 29. |
| 4. | Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na elimu ya kati kwani bajeti na idadi ya wanufaika imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka jambo ambalo ni jema sana. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo kwa ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa wanaostahili pamoja na Bodi kushindwa kupata marejesho ya mikopo kwa wanufaika. Kamati inatoa maoni yafuatayo:<br>(i) Kwa kuwa, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imeongezewa | (i) Serikali imepokea ushauri.<br>Hata hivyo, Serikali imekuwa ikiongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kila mwaka kwa kuzingatia upatikanaji wa rasilimali fedha. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitatu, bajeti ya mikopo imeongezeka kutoka **Shilingi 570 bilioni** mwaka **2021/22** hadi **Shilingi bilioni 786** mwaka **2023/24** ambazo zilijumuisha **Shilingi bilioni 48** za mikopo ya elimu kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi stadi (maarufu vyuo vya kati) iliyoanza kutolewa mwaka 2023/24. Kwa mwaka wa fedha 2024/25, **Shilingi bilioni 787** imetengwa kwa ajili ya kutoa mikopo, |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | jukumu la kutoa mikopo ya elimu ya kati, Serikali iongeze bajeti ya Bodi ya Mikopo kwa ajili ya kuongeza idadi ya wanafunzi wa elimu juu na elimu ya kati wanaostahili kupata mikopo. | ambapo hadi Februari, 2025 Serikali imetoa mikopo kwa wanafunzi 87,251 wa mwaka wa kwanza ambapo shahada ya kwanza 81,079 na Shahada za juu 307 (stashahada ya uzamili 200, Umahiri 88 na Uzamivu 20). Aidha, imetoa mikopo kwa wanafunzi 161,080 wanaoendelea na masomo ambapo shahada ya kwanza 157,937 na Shahada za juu 61 (Umahiri 21 na Uzamivu 40). Vilevile, imetoa ufadhili kwa wanafunzi 674 wa mwaka wa kwanza na 669 wanaoendelea kupitia SAMIA Skolashipu. Mikopo ya elimu kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi (maarufu vyuo vya kati) imetolewa kwa wanafunzi 5,138 wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 2,369 wanaoendelea wa ngazi ya stashahada katika fani za sayansi na ufundi.<br>Aidha, Serikali imeingia |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | makubaliano na taasisi za kifedha ikiwemo Benki ya NMB kwa ajili ya kutoa mikopo ya riba nafuu ya elimu hatua ambayo itaendelea kuimarisha fursa za kuongeza wanufaika wa mikopo katika ngazi ya elimu ya kati na elimu ya juu ambapo hadi Septemba, 2024 NMB imetoa mkopo kwa wahitaji 68 yenye jumla ya Shilingi **29,000,000.00**. |
| | (ii) Kamati inasisitiza kuwa, Serikali iangalie upya vigezo vya utoaji wa mikopo ya Elimu ya Juu ili kupunguza malalamiko ya kutokuwa na vigezo vya ulinganifu yanayojitokeza mara kwa mara miongoni mwa waombaji na wazazi; | (ii) Serikali imepokea ushauri. Serikali kupitia Bodi ya Mikopo inaendelea kutoa mikopo kwa kuzingatia vigezo vinavyotajwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo Sura 178 ikiwemo mwombaji: Awe Mtanzania; Awe ameomba mkopo; Asiwe na chanzo kingine kinachogharimia masomo yake na awe amewasilisha maombi ya mkopo kwa kuzingatia taratibu na mfumo uliowekwa. Aidha, kipaumbele hutolewa kwa makundi maalum ya wahitaji ambao ni yatima, wenye |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | ulemavu na waliofadhiliwa katika masomo yao kabla ya kujiunga na elimu ya juu. Pamoja na utaratibu huu katika mwaka 2023/24, Serikali imekamilisha mapitio ya Muundo na Utendaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na kuboresha vigezo ambavyo vitaanza kutumika kuanzia 2025/26 baada ya kuridhiwa na wadau. |
| | (iii) Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu iongeze juhudi ya kutoa elimu kwa umma hususan umuhimu na ulazima wa wanafunzi waliopata mikopo hiyo kurejesha fedha hizo kama sheria inavyoelekeza; | (iii) Serikali imepokea ushauri. Serikali inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu urejeshaji wa mikopo kwa hiari. Vilevile, imewezesha kusomana kwa mifumo ya TRA na NSSF ambayo imeongeza ufanisi wa Bodi ya Mikopo kupata taarifa za wanufaika waliopo katika sekta binafsi. Hivyo, pamoja na jitihada nyingine kuunganishwa kwa mifumo hiyo kumewezesha kuwabaini wanufaika kutoka 40,000 hadi 54,000. Vilevile, Serikali imeendelea kuwa na |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | kampeni ya urejeshaji wa mikopo iliyoiva kupitia vyombo vya habari zinazolenga kutoa hamasa kwa wanufaika wenye kipato ambao hawajaanza kurejesha mikopo. Mfano wa kampeni hizo ni pamoja na Sifurisha (2021/2022 -2022/2023) na Fichua (2023/2024) na kampeni hizo zinaendelea. |
| | (iv) Bodi ya Mikopo iangalie namna ya kuweka utaratibu madhubuti wa kurahisisha utoaji wa mikopo na ukusanyaji wa mikopo ndani na nje ya nchi ili mikopo hiyo iweze kuwakopesha wengine. | (iv) Serikali imepokea ushauri. Katika kurahisisha utoaji wa mikopo na ukusanyaji wa mikopo ndani na nje ya nchi, Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya Bodi ya mikopo ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa mikopo wakati wote. Aidha, kwa kuzingatia miongozo ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (*e-Government Authority*), hadi Mei, 2024, HESLB imeunganisha mifumo ya TEHAMA na wadau wa kimkakati kama TASAF, RITA, TCU, NACTVET, NECTA na ZHELB. HESLB. imewezesha kusomana |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | kwa mifumo ya TRA, NIDA, ATE na NSSF ambayo imeongeza ufanisi wa Bodi ya Mikopo kupata taarifa za wanufaika waliopo katika sekta binafsi. Hivyo, pamoja na jitihada nyingine kuunganishwa kwa mifumo hiyo kumewezesha kuwabaini wanufaika kutoka 40,000 hadi 54,000. |
| 5. | Katika kuanza utekelezaji wa Mtaala mpya wa Elimu na kusisitiza mafunzo ya Amali, Kamati imebaini uwepo wa upungufu wa rasilimali fedha pamoja na miundombinu jambo ambalo linaweza kuathiri madhumuni ya mtaala mpya na kwamba inaweza kuathiri manufaa ya Elimu waipatayo wanafunzi. Hivyo, basi Kamati inashauri yafuatayo:<br><br>(i) Serikali iongeze bajeti | (i) Serikali imepokea ushauri.<br><br>Serikali inatambua umuhimu wa kutekeleza mitaala iliyoboreshwa kwa ufanisi. Ili kufikia azma hii, kwa mwaka wa fedha 2024/25 Serikali imetenga fedha jumla ya **Shilingi 202,603,947,343.00** kwa ajili kuwezesha utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa katika maeneo yafuatayo:<br><br>a. Mafunzo kabilishi kwa walimu **Shilingi 17,476,241,202.00;**<br>b. Ujenzi wa miundombinu |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| | kwa ajili ya utekelezaji wa mitaala mipya pamoja na kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia kama vile kujenga Karakana, Maabara pamoja na kuhakikisha vifaa vya mafunzo ya amali vinapatikana. | **Shilingi 132,250,916,334.00;** na<br>c. Vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo Vitabu **Shilingi 52,876,789,807.00.**<br><br>Vilevile, hadi kufikia Februari, 2025 **Shilingi 34,302,923,680.92** zimetumika kwa ajili ya mafunzo kwa walimu 86,709 na **Shilingi 411,490,493,707.66** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo Shule za Sekondari za Amali 103, Shule za Sekondari za Kata 234, Shule za Msingi mpya 78, Madarasa 1875 katika shule za msingi na madarasa 596 katika shule za sekondari, mabweni 971 na nyumba za walimu 302 na matundu ya vyoo 9,086. Aidha, Serikali itaendelea kuongeza bajeti kadri ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa. |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | Serikali iongeze fedha kwa ajili ya vyuo vya ualimu ambavyo vitatoa na kuandaa mafunzo ya ualimu yanayoendana na mtaala mpya. | (ii) Serikali imepokea ushauri.<br><br>Itaendelea kuongeza bajeti kwa ajili ya vyuo vya ualimu kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha ili kutekeleza kwa ufanisi mitaala iliyoboreshwa hususani mafunzo ya ualimu. |
| 6. | Utaratibu uliopo wa kuchapisha vitabu kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi ni kuwa Wizara ya Fedha inapeleka fedha Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambao nao wanapeleka fedha hizo Taasisi ya Elimu Tanzania kupitia Wizara ya Elimu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, **Shilingi Bilioni 17** zilizopelekwa TAMISEMI tangu mwezi Novemba, 2023, zilikaa hadi mwezi Machi 2024 takribani miezi 5 bila | Serikali imepokea ushauri.<br><br>Serikali itaweka utaratibu kuwezesha Taasisi ya Elimu Tanzania kupata fedha kwa wakati ili kutekeleza jukumu la kuandika, kuchapa, na kusambaza vitabu kwa ufanisi. Aidha, majadiliano kati ya WyEST, OR – TAMISEMI na HAZINA yamefanyika kupitia vikao na uwasilisha wa barua (Kumb.Na. HA.18/162/01M/37 ya tarehe 16 Januari, 2024 na Kumb. Na. HA.216/229/01E/6 ya tarehe 03 Machi, 2025 ya kuomba kuhamisha bajeti ya fedha |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | kutumika. Suala la fedha hizo kukaa kwa muda mrefu TAMISEMI na kutokutumika kama ilivyokusudiwa limesababisha fedha kurejeshwa Hazina ingawa Taasisi ya Elimu Tanzania ilikuwa inahitaji fedha hizo kwa ajili ya uchapishaji wa vitabu.<br>Kamati inasikitishwa na hali hii inayoendelea kwani inakwamisha azma ya utekelezaji wa mtaala mpya ambao umeanza kutekelezwa mwaka, 2024 hivyo kusababisha watoto kukosa vitabu bila sababu za msingi na kusababisha kuchelewa kwa taratibu za manunuzi, uchapaji na usambazaji wa vitabu shuleni unaoathiri ujifunzaji na ufundishaji.<br>Kamati inaishauri Serikali | kwenye Fungu 46 – WyEST na kwa mwaka wa fedha 2025/26 fedha hizo zimezingatiwa katika Fungu 46.<br><br>Wizara inaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kwa jitihada zake katika kuhakikisha Fedha za Ununuzi wa Vitabu kutoka Fungu 56 (OR – TAMISEMI) zinahamishiwa Fungu 46 (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia). |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | kuwa, kwa kuwa jukumu la kuandika, kuchapa, na kusambaza vitabu linatekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), ni vema fedha za uchapishaji wa vitabu zipelekwe TET moja kwa moja kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ili kuongeza ufanisi, kasi na kufikia malengo ya Wizara katika uandaaji na usambazaji wa vitabu shuleni. | |
| 7. | Kwa kuwa mafunzo ya ualimu kazini ni sehemu muhimu ya kuboresha ustadi wa ufundishaji na kuhakikisha walimu wanakidhi mahitaji ya wanafunzi katika mazingira ya kisasa ya elimu kulingana na mitaala mipya. Na kwa kuwa, | Serikali imepokea ushauri.<br>Serikali imetoa mafunzo ya mtaala ulioboreshwa kwa walimu wanaofundisha darasa la Awali mpaka la saba ambao idadi yao ni 181,777 (shule za msingi za Serikali ni 155,476 na zisizo za Serikali ni 26,301). Aidha, Mafunzo hayo yamehusisha pia walimu wakuu, wathibiti wakuu ubora wa |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| | mafunzo hayo bado utekelezaji wake siyo wa kuridhisha. Hivyo basi, ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa mtaala mpya, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha walimu wote wanapaswa sio tu kuufahamu vizuri Mtaala huu lakini pia kujengewa uwezo wa mafunzo ya namna bora ya utekelezaji wa mtaala mpya ili waweze kuboresha ujuzi na kupata mbinu mbalimbali za ufundishaji ambazo zitasaidia kujifunza maarifa mapya. Aidha, Mafunzo haya yatolewe kwa walimu wote nchini wa Shule za Msingi na Sekondari. | shule, maafisa elimu kata, maafisa elimu halmashauri, maafisa elimu mikoa na maafisa elimu taaluma wa halmashauri na mikoa.<br>Aidha, Mwaka 2022 wizara iliandaa miongozo minne ya uendeshaji wa mafunzo endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) kwa lengo la kutoa utaratibu wa namna ya uendeshaji wa mafunzo ya walimu kazini. Miongoni mwa taratibu zilizoanzishwa ni utoaji wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) katika ngazi ya shule na Vituo vya walimu. Kwa kuzingatia utaratibu huu, mafunzo ya walimu kazini yataendelea kutolewa na Serikali na yatawafikia walimu katika ngazi ya shule na vituo vya walimu.<br>Katika mwaka wa fedha 2024/25 imetoa mafunzo kuhusu utekelezaji wa mtaala ulioboreshwa wa ngazi ya Elimu ya msingi na sekondari kwa walimu 287,108 wa shule za Serikali na |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | | zisizo za serikali. |
| 8. | Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za nje unaotokana na ukomo mdogo wa fedha ambao unachangia kwa kiasi kikubwa kuchelewesha utekelezaji wa miradi hiyo na hivyo kusababisha kusuasua kwa baadhi ya miradi. Kamati inaishauri Serikali kuwa, vifungu vya fedha za nje vinavyotekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia vitanuliwe bila kuathiri Sheria, Kanuni na Taratibu za matumizi ya fedha za Serikali ili zitekeleze miradi iliyokusudiwa. | Serikali imepokea ushauri.<br>Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali imeongeza ukomo wa bajeti kwa fedha za nje kutoka **Shilingi 158,788,000,000.00** mwaka 2023/24 hadi kufikia **Shilingi 294,649,005,000.00** mwaka 2024/25 kwa lengo la kuruhusu matumizi ya fedha za miradi ya nje. Aidha, **Shilingi 265,264,177,075.54** zimeombwa HAZINA kwa ajili ya kutanua vifungu vya matumizi ya fedha za nje za maendeleo baada ya kumaliza tengeo la bajeti la mwaka 2024/25. |
| 9. | Kumekuwepo na ongezeko kubwa la | Serikali imepokea ushauri.<br>(i) Serikali inatambua uwepo wa |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | mdondoko wa wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari hususani watoto wa kiume, hali inayopelekea ongezeko kubwa la watoto wa kiume kuwepo mtaani. Kamati imebaini mdondoko huo unasababishwa na Watoto wa kiume kutopewa mkazo wa masomo kama ilivyokuwa kwa watoto wa kike. Aidha, sababu nyingine zinazosababisha ongezeko la mdondoko huo ni ajira za utotoni kwa baadhi ya wanafunzi huchagua kuacha shule ili kusaidia familia zao kwa kufanya kazi au shughuli za kiuchumi na kushindwa kitaaluma. Hivyo basi, Kamati inatoa ushauri ufuatao:<br>(a) Serikali iweke mkakati madhubuti wa | changamoto ya mdondoko wa wanafunzi wa kiume katika shule za msingi na sekondari. Kutokana na hali hii, Serikali imeongeza shule za bweni za wavulana kama ilivyokuwa kwa wasichana. Mwaka 2024/25 **Shilingi bilioni 28.7** zimetumwa katika halmashauri kwa ajili ya kujenga shule 7 za kanda za wanafunzi wa bweni (wanafunzi 1,200 kwa kila shule). Shule hizi zinajengwa Mkoa wa Pwani, Dodoma, Lindi, Songwe, Simiyu, Katavi na Manyara.<br>Vilevile, jitihada mbalimbali zinafanyika ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaoandikishwa wanamaliza mzunguko wao wa elimu. Serikali kupitia programu ya shule salama imetekeleza yafuatayo:<br>a) Mpango wa chakula shuleni; |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | kuhakikisha wanafunzi wote walioandikishwa shule wanahitimu masomo yao. Aidha, Waraka uliotumika kuwarudisha watoto wa kike shuleni utumike pia kuwarudisha watoto wa kiume shuleni. Vilevile, walimu wapewe mafunzo ya kufundisha watoto waliopo nje ya mfumo rasmi; | b) Mpango wa ushirikiano wa wazazi na walimu ili kuhakikisha watoto wanakuwa shuleni katika muda wote wa masomo;<br>c) Kuhakikisha ulinzi na usalama kwa watoto wote wawapo shuleni;<br>d) Mafunzo ya elimu rika, stadi za maisha, na masuala ya jinsia kwa wanafunzi;<br>e) imetoa mafunzo kuhusu utoaji wa huduma ya ushauri na unasihi, haki na uundwaji wa dawati la malalamiko shuleni kwa walimu wa shule za msingi na sekondari 104,244; na<br>f) Uwepo wa utaratibu wa Wathibiti Ubora wa Shule kufuatilia kuwa wanafunzi walioandikishwa wanamaliza mzunguko |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| | | wao wa elimu.<br>Aidha, Waraka wa Elimu Na. 2 wa Mwaka 2021 na Mwongozo wake wa Mwaka 2022 vinatoa fursa kwa wanafunzi wote ikiwemo wa kiume waliokatiza masomo katika Elimu ya Msingi na Sekondari kwa sababu mbalimbali kurejea ili waweze kukamilisha mzunguko wao wa elimu. Hadi kufikia Februari 2025, wavulana 5,613 (msingi 4,041 na sekondari 1,572) na wasichana 10,239 wa sekondari wamerejea katika mfumo rasmi wa elimu.<br>Vilevile, Wizara itaendelea kutenga bajeti ya kuwajengea uwezo wa kuwafundisha wanafunzi/watoto walioko nje ya mfumo rasmi kadri ya mahitaji yatakavyojitokeza. Katika kutekeleza hilo, katika mwaka wa fedha 2022/23 wizara iliwajengea uwezo walimu 1,854 wanaofundisha wanafunzi wanaosoma nje ya mfumo rasmi |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- | --- |
| | | kupitia mpango wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA). Katika mwaka 2024/25 wizara imewajengea uwezo walimu 599 wa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi. |
| | (ii) Waraka uliotolewa na Mhe. Rais *(Re-entry)* wa kuwarudisha wanafunzi wa kike waliokatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali uingizwe katika marekebisho ya Sheria ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa kuwa Sheria iliyopo sasa haina kipengele hicho. | (b) Serikali imepokea ushauri. Waraka Na. 2 wa Mwaka 2021 wa Kuwarejesha Wanafunzi Walioacha Shule kwa sababu mbalimbali na Mwaka 2022, na Mwongozo wa kuwarejesha wanafunzi waliokatiza masomo shule ya msingi na sekondari kwa sababu mbalimbali. utazingatiwa katika mapitio ya Sheria ya Elimu ambapo yataweka masharti ya utekelezaji wa Waraka na Mwongozo huo. |
| 10. | Malengo ya kuanzishwa kwa Vyuo Vikuu nchini ni kutoa elimu ya juu yenye ubora, kukuza tafiti na uvumbuzi, kukuza ujuzi na | Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha miundombinu katika vyuo vikuu nchini. Katika mwaka wa fedha 2023/24 Serikali inaendelea na ujenzi wa Ndaki ya |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | stadi, kusaidia na kuchochea maendeleo ya kitaifa na kukuza utamaduni na maadili katika jamii. Licha ya kazi nzuri inayofanywa na vyuo hivi, Kamati inaamini kuwa, Vyuo Vikuu vina wajibu wa kuhakikisha vinatoa mchango wake kwa kuendeleza na kukuza viwango vya elimu na mafunzo nchini ili kupata rasilimali watu yenye weledi, maarifa na ujuzi katika nyanja mbalimbali kwa maendeleo ya Taifa.<br>Kamati inaona upo umuhimu wa Vyuo Vikuu kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia malengo ya uanzishwaji wake ambavyo ni alama katika nchi yetu kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha | Sayansi za Ardhi na Uhandisi (CoESE) ambapo ujenzi umefikia **asilimia 18.75** na Ndaki ya Sayansi Asilia na Hisabati (CNMS) ambapo ujenzi umefikia **asilimia 7.5** katika Chuo Kikuu cha Dodoma ambapo **Shilingi 25,613,384,160.47** zilitengwa. Lengo la Serikali ni kuendelea kutenga fedha za kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika majengo ya Ndaki hizo ili yatumike kwa lengo lililokusudiwa. Vilevile, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 6.5** kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya Chuo kikuu cha Dar es Salaam.<br>Aidha, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu mbalimbali ya vyuo vikuu kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha. Hadi Februari 2025 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimetumiwa **Shilingi 5,348,002,309.00** na Chuo Kikuu cha Dodoma **Shilingi 6,464,286,563.64** |

| NA | MAONI NA USHAURI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| | Dodoma. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kwamba, Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kiendelee na utekelezaji wa malengo yaliyowekwa ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa Kampasi ya Sayansi Asilia (Natural Science Campus) kama ilivyokusudiwa. Kwa upande wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kihakikishe ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali inayoendelea kutekelezwa ikamilike kwa wakati. | |